JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU,

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO

*Unapojibu tafadhali taja:*

**Kumb: Na. AB.113/388/01/76** **Tarehe: 27 Januari, 2026**

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi wa Manispaa ya Ubungo anawatangazia Watanzania wenye sifa kuomba nafasi za kazi **(4)** za mkataba wa muda mfupi katika Manispaa ya Ubungo kwa ajili ya kuendesha Mtambo wa kuchonga na kuumba barabara (**Greda**), Mtambo wa kuchimba na kupakia (**Excavator**) na Mtambo wa kushindilia (**Roller**).

### 1.0 DEREVA MITAMBO DARAJA LA II - NAFASI NNE (04)

### 1.0.1 KAZI NA MAJUKUMU

i. Kuendesha Mitambo chini ya Usimamizi wa Dereva wa Mitambo wenye uzoefu.

ii. Kufanya Usafi wa Mitambo.

iii. Kufanya Matengenezo madogo madogo ya Mitambo

iv. Kukagua kabla na baada ya kuendesha Mitambo.

v. Kufanya Kazi nyingine kadiri atavyoelekezwa na Msimamizi na atakazopangiwa na Mwajiri.

### 1.0.2 SIFA ZA MWOMBAJI

i. Awe na elimu ya kidato cha nne au sita.

ii. Awe na Leseni Daraja la G ya kuendesha mitambo.

iii. Awe na uwezo wa Kuendesha Mtambo na Ujuzi wa Kutunza vyombo mbalimbali vya mitambo hiyo.

iv. Awe na uzoefu wa kuendesha Mitambo kwa muda usiopungua masaa miatatu (300) au miezi mitatu bila kusababisha ajali.

v. Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya Uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha VETA au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.

### 1.1.2 NGAZI YA MSHAHARA

**Kwa kuzingatia viwango vya mishahara ya serikali mshahara utakuwa ngazi ya TGOS "A" kwa mwezi**

**MASHARTI YA JUMLA.**

i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania, wenye umri wa kuanzia miaka18 na usiozidi miaka 45.

ii. Waombaji waambatanishe Cheti cha Kuzaliwa,

iii. Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye Anuani, Namba za Simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (Referees) wa kuaminika,

iv. Waombaji wote waweke nakala za vyeti vya taaluma na vyeti vya Kidato cha Nne na Sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika

v. Waombaji kazi wa Kada ya kuendesha mitambo wenye leseni Daraja G wanapaswa **KUAMBATISHA** vyeti vya mafunzo ya kuendesha mitambo vilivyowapatia sifa ya kupata madaraja husika.

vi. Waombaji wote waweke picha mbili *"Passport Size"* ya hivi karibuni.

vii. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali kutoka kwa Katibu Mkuu Kiongozi,

viii. Waombaji wenye majina tofauti katika vyeti vya Taaluma, Kuzaliwa na NIDA waambatishe **DEED POLL**

ix. Uwasilishwaji taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria,

x. Kwenye barua ya maombi ainishe aina ya mitambo anayoweza kuendesha kati ya mitambo iliyoorodheshwa hapo juu.

xi. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **10 Februari, 2026.**

**MUHIMU:** *Kumbuka kuambatanisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya Elimu, na Maombi yote yatumwe kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo kwa kuleta maombi moja kwa moja kupitia Anuani hii*

**Mkurugenzi wa Manispaa,**
**Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo,**
**S.L.P. 55068,**
**Ubungo - Dar Es Salaam.**

**Limetolewa Na: -**

..........................

Dkt. Aron T. Kagurumjuli

**MKURUGENZI WA MANISPAA**

MKURUGENZI WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO
DAR ES SALAAM